**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU**

**NAMBA ZA SIMU**

**MKUU WA SHULE: 0622613625**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0625652900**

**SHULE YA SEKONDARI: MURRAY**

**S. L. P 48,**

**MBULU,**
**MANYARA**

**TAREHE:……………………**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………………………………………………

S. L. P …………………………………………………………………………………………………………………………….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MURRAY HALMASHAURI YA MJI WA MBULU MWAKA…………….

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha

Tano katika shule hii mwaka……………. na atasoma tahasusi ya ……………………………

Shule ya Sekondari **Murray** ipo umbali **wa kilometa 18** kusini mashariki mwa mji wa

**Mbulu**. Usafiri wa Cruser kutoka Mjini Mbulu unapatikana katika kituo cha mabasi

**MBULU mjini** Nauli ni **shilingi elfu 4,000/-** land cruser, na **6,000 pikipiki** inayopatikana **sheli ya chini** barabara ya kuelekea hospitali ya mji wa mbulu..

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………………………Mwisho wa kuripoti

Ni tarehe **……………………………………..**.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

Sare za shule

**(A) WASICHANA**

i) Sketi rangi ya kijani pea mbili. Utajishonea, inayoishia chini ya magoti itakayovaliwa juu ya suruali.

ii)suruali rangi ya kijani pea mbili itakayovaliwa ndani ya sketi

iii) Shati nyeupe (Halwa) yenye mikono mirefu pea mbili- utajishonea /kujinunulia

iv) Tai ndefu ragi ya kijani.

v) Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vi) Sweta 1 rangi ya kijani shingo V

vi) Aje na T-shirt rangi ya damu ya mzee yenye Colar .

(anaweza kuinunua shuleni kwa shilingi 15,000/=

viii) Rangi ya Hijab (Kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi, pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

ix) Sare za michezo- Track suti rangi ya bluu iliyokolea, tisheti 1 ya njano isiyo na maandishi yeyote, shingo duara na raba nyeusi pea mbili ( ajinunulie).

x) Viatu vya shule pea mbili vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

xi) Tracksuti 1 ya rangi ya kijivu yenye mistari mweupe kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea.

xii) Sketi 1 ya kazi (shamba dress) rangi ya dark blue mshono marinda chini ya magoti iwe ndefu kwa ajili ya kazi za nje na T-shirt rangi ya njaro yenye colar.

3**. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i) Madaftari 10 (counter book Q4), kalamu za kutosha, Rula, mathematical set, Scientific calculator, **Ream mbili (A4)** kwa mwaka na Dissecting Kit kwa mwanafunzi wa Masomo ya sayansi (CBG).

ii) Mwanafunzi kwa TAHASUSI yake anashauriwa kujinunulia vitabu vya ziada na kiada.

(Atashauriwa na mwl. Wake wa somo hata baada ya kuripoti)

iii)Barua ya kuripoti (Joining instruction)

iv) Vyeti vyako (vivuli vya vyeti) vya kidato cha nne (form iv) Academic, Leaving certificate na cheti cha kuzaliwa.

v) Cheti cha daktari (medical Examination Certificate) ambacho kimejazwa vizuri na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali

vi) Fomu ya makubaliano ya mzazi kumsomesha mwanae (fomu zimeabatanishwa nyuma ya barua hii).

vii) Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya blue bahari.

viii) Mashuka jozi 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1 nzito, chandarua 1 ya mstatili rangi ya blue.

ix) Taulo (1), nightdress

x) Mwavuli 1, buti ya matope kwa ajili ya shughuli za nje wakati wa mvua.

xi) Aje na Godoro inchi 3 kwa futi 2.5- (futi mbili na nusu).

xii) Vyombo vya chakula:- Sahani ya bati, kikombe, bakuli na kijiko ( vyote aluminium)

xiii) Sanduku la bati/Chuma la kufunga kwa kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako.

xiv) Mwanafunzi aje na **BIMA** ya Afya kwa ajili ya matibabu yake au aje na Tsh**. 50,400/=**

xv) **NB:** Gharama nyingine ya dawa nje ya bima atagharimia mzazi, shuleni tunatoa huduma ya kwanza tu.

xvi) Ndoo mbili (2) yenye ujazo wa lita 10 zenye mifuniko kwa matumizi yake binafsi

xvii) Jembe 1 lenye mpini imara kwa ajili ya kazi za shule.

xviii) Mopa1, kwanja/ fyekeo 1, ufagio wa chelewa 1, soft au hard broom 1 kwa ajili ya kufanyia usafi.

xix) Nguo za ndani za kutosha

***MUHIMU: Ili kumpunguzia Mzazi/mlezi gharama za kusafiri na mizigo mingi, shule inapenda Kukujulisha kuwa vifaa vingi anavyotakiwa kuja navyo mwanafunzi kama vile Ream, jembe, Ndoo, fyekeo, mopa, fagio, chelewa, n.k vinapatikana maeneo ya shule kwa gharama ya sokoni.***

4. Michango mbalimbali:-

| Na. Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|
| 1. Mchango wa uendeshaji wa shule | 75,000/= |
| 2. Tahadhari | 5,000/= |
| **Jumla** | **80,000/=** |
| | |

NB: Fedha zilipwe Benki Kwa Ac. Na. **41210015239. Jina Akaunti ya wazazi murray sekondari.**

Utakapofika shuleni unatakiwa kuwasilisha “**bank pay-in slip**” kwa mhasibu wa shule ili akuandikie stakabadhi ya malipo.

Kila mwanafunzi atagharimia mahafali mwaka kwa mwaka na uchapishaji wa cheti ADVANCED LEAVING CERTIFICATE) mwaka wa mwisho wa masomo yake.

## 5. Sheria na kanuni muhimu za shule

**S**hule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa Kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa Nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:-

## 6. Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa kwa ujumla ni jambo la lazima;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu Masomo ya usiku (preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

x) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na hakuna Mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa shule. (kwa msiba au ugonjwa)**.

## 7. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule;
vi. Kusuka nywele;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya kimapenzi, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha matendo ya uhalifu,siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu; n.k.
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**8. Viambatisho na Fomu Muhimu**

**i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (medical Examination form)** ambayo itajazwa **na Mganga Mkuu wa** Hospitali ya serikali;

**ii)** Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu Historia ya mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa shule…………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule:……………………………**

**Mhuri wa Mkuu wa shule ……………………………………………………………………………**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).**

**Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na**

**Watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi**

**husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuu wa shule**
  - **. 0622613625 Mkuu wa shule**
  - **. 0625652900 Makamu Mkuu**
  - **. 0622452857 mwalimu taaluma**

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATIONB FORM)**

**AMBAYO ITAJAZWA NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Wilaya)
-------------------------------------------------------------------------------- Ninathibitisha
Kuwa mwanafunzi huyu ( jina la mwanafunzi)
…………………………………………………………………… Amepimwa nami kikamilifu na
Kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

(a) HALI YA MWILI:-

(i) Mapigo ya Moyo…………………………………………………………………………………………..
(ii) Haemoglobin (HB) ……………………………………………………………………………………
(iii) Kundi la damu (blood group) ……………………………………………………………………….
(iv) Mkojo (Urine) ……………………………………………………………………………………………..
(v) Kinyesi (stool) ……………………………………………………………………………………………
(vi) Macho (Eye) ……………………………………………………………………………………………….
(vii) Masikio (Ear) ……………………………………………………………………………………………

Angalia:- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i) – (vii)

(b) MAGONJWA:-
> Amewahi/hajawahi/ana/hana magonjwa yafuatayo:-

(a) Pumu
…………………………………………………………………………………………………………………

(b) Kifua kikuu

……………………………………………………………………………………………………………………

(C) Kifafa

……………………………………………………………………………………………………………………

(d) Shinikizo la damu chini/ juu

…………………………………………………………………………………………………………………….

e) Vidonda vya tumbo

……………………………………………………………………………………………………………………

f) Maradhi ya zinaa

………………………………………………………………………………………………………………………………………

g) Ukoma

………………………………………………………………………………………………………………………………………

h) Mental illness (ugonjwa wa akili)……………………………………………………...........................

i) maradhi mengiye yasiyotajwa hapo juu.

………………………………………………………………………………………………………………………………………

SAHIHI NA MHURI WA DAKTARI/MGANGA

TAREHE ………………………………………………….

FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA

MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE

SEHEMU A (Ijazwe na mwanafunzi

1. Jina la mwanafunzi (Majina matatu)

……………………………………………………………………………

2. Uraia

………………………………………………………………………………………………………………………………..

3. Tarehe ya kuzaliwa

…………………………………………………………………………………………………………..

4. Shule anayotoka

………………………………………………………………………………………………………………

5. Tarehe ya kutoka shule hiyo

……………………………………………………………………………………………….

SEHEMU B. (Ijazwe na mzazi/mlezi)

1. Jina la mzazi/mlezi (Majina matatu) ……………………………………………………………………………………

2. Anuwani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………………………………….

3. Mahali anapoishi ………………………………………………………………………………………………………………..

4. Mawasiliano ya mzazi/mlezi (Namba ya simu) …………………………………………………………………

5. Kazi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………………………………………….

Mahali anapofanya kazi ……………………………………………………………………………………………………….

6. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi)

**NB: Mwanafunzi atatembelewa Jumamosi ya mwisho wa mwezi**.

Jina la Ndugu wa 1 ……………………………………………….. Namba ya simu ………………………
Anuwani yake ………………………………. Uhusiano wake ………………………………….
Jina la ndugu wa II: ……………………………………. Namba ya simu……………………………….
Anuwani yake ………………………….. Uhusiano wake…………………………

TAREHE …………………………… SAHIHI YA MZAZI/MLEZI …………………………………………..

FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUMSOMESHA

MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………….. wa kijiji cha ……………………………………………………….

Kata ya …………………………………………….. Halmashauri ya ………………………………………………………………….

Ambaye ni mzazi/mlezi wa ………………………………………………………………………………………………………….

Anayeingia kidato cha ………………..... Katika shule sekondari **Murray**

Najifungia wajibu huu kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi tajwa hapo juu mbele ya utawala

Kijiji changu hiki. Nimesoma barua ya kumwita shuleni,sheria za shule na fomu zote

Zilizoambatishwa, nimeelewa kila kitu na kuridhika. Pia najua nisipotimiza mashartii yote

Mwanafunzi huyu hatapokelewa shuleni. Nakubali ahadi hiyo nikijua ni ahadi ambayo

Sitaweza kuikiuka bila hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.

Sahihi ya mzazi au mlezi ………………………………………………... Tarehe …………………………………..

Sahihi ya afisa mtendaji …………………………………Tarehe……………….. Namba ya simu………………………….